JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

UUNDAJI, USAJILI NA UENDESHAJI WA VYOMBO VYA

WATUMIAJI MAJI (COWSOs)

Machi 2017

YALIYOMO:-

1. **UTANGULIZI**
2. **TARATIBU NA HATUA ZA UUNDAJI WA JUMUIYA YA WATUMIAJI MAJI (*COWSO*)**
3. **USAJILI WA *COWSO***
4. **MAKABIDHIANO YA CHETI**
5. **FAIDA ZA KUSAJILI *COWSO***
6. ***6.*** **MAJUKUMU YA *COWSO***
7. **UENDESHAJI WA JUMUIYA YA WATUMIAJI MAJI**
8. **HITIMISHO**
9. **VIAMBATISHO**

1. UTANGULIZI

Dhana ya kuunda na kusajili *COWSO* (*Community Owned Water Supply Organisation)* ni kuimilikisha miradi ya maji kwa Watumiaji maji ili wajisikie kuwa ni mali yao.

Lengo: Wananchi kumiliki, kusimamia uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini kisheria ili utoaji wa huduma uweze kuwa endelevu kama Sera ya Maji ya mwaka 2002 inavyoelekeza.

2.0 TARATIBU NA HATUA ZA UUNDAJI WA VYOMBO VYA WATUMIAJI MAJI (COWSOs)

COWSO itaundwa baada ya wananchi kukubaliana kwa pamoja kwa kuzingatia masharti au vigezo vinavyoendana na Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya mwaka 2009.

Zifuatazo ni taratibu na hatua za uundaji wa *COWSO* :-

- Kamati ya maji na usafi wa Mazingira ya kijiji kwa kushirikiana na CWST wataitisha kikao cha awali kati yao na Viongozi/Wajumbe wa serikali ya Kijiji ili kuuza wazo.
- Viongozi/Wajumbe wa Serikali ya Kijiji na Kamati ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Kijiji wakishaafikiana uamuzi utawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji.
- Katika Mkutano Mkuu wa Kijiji *CWST* watawaelimisha wananchi kuhusu:-
- Sera ya Maji ya mwaka 2002,
- Aina za vyombo vya watumiaji maji (Faida na hasara),
- Taratibu na hatua za kuunda, kusajili *COWSO*
- Kamati ya muda itateuliwa kwa kuzingatia uwakilishi wa vituo vya kuchotea maji au vitongoji kwa vijiji ambavyo havina mradi bado.
- Rasimu ya katiba itaandaliwa na kamati ya muda kwa kushirikisha Mwanasheria wa Halmashauri husika.
- Rasimu ya katiba na kanuni kuwasilishwa kwenye mkutano wa kijiji (village assembly) ili kujadiliwa na kupitishwa.
- Kamati ya muda itawasilisha rasimu ya katiba na kanuni ili kuhakikisha kutokuwepo kwa pingamizi ndani ya kata na kupata ridhaa. Hii itawezesha kubaini kuwepo au kutokuwepo kwa jumuiya kama ile inayopendekezwa.
- Kamati ya muda, mwenyekiti na Mtendaji wa serikali ya kijiji watawasilisha rasimu ya katiba pamoja na Kanuni, Muhtasari wa mkutano yakiwemo majina ya waliohudhuria na sahihi zao kwa Mkurugenzi mtendaji.
- Kufikia hatua hii, *COWSO* tayari itakuwa imeundwa kulingana na katiba na kanuni.
- Nafasi 3 za Uongozi wa juu zitatangazwa (Mwenyekiti, Katibu na Mhazini). Iwapo mjumbe wa Kamati ya muda ataomba nafasi ya Uongozi itabidi uanakamati wake usitishwe. Viongozi watachaguliwa Kidemokrasia na wananchi kwa kuzingatia asilimia 50 au zaidi kuwa wanawake kila baada ya miaka mitatu na watakuwa Wajumbe wa Kamati tendaji.
- Baada ya Jumuiya kuundwa na viongozi kupatikana Kamati ya Muda itakabidhi shughuli na nyaraka zote za utendaji kwa Viongozi waliochaguliwa rasmi ili waendelee na zoezi la usajili. Kamati ya muda itafikia ukomo katika hatua hii.

3. TARATIBU NA HATUA ZA USAJILI WA JUMUIYA YA WATUMIAJI:-

Zifuatazo ni hatua za kusajili Jumuiya ya Watumiaji Maji zitakazofanywa na Kamati Tendaji baada ya kuundwa:-

- Barua ya maombi ya kusajili Jumuiya ikiambatanishwa na katiba, kanuni, Muhtasari saini zao, na sifa za viongozi wa kudumu itapelekwa Halmashauri.
- Wananchi watafahamishwa iwapo maombi yao hayajafuzu vigezo vilivyowekwa au kama yanahitaji maboresho kabla ya kusajiliwa.
- Maombi yaliyokubalika pamoja na nyaraka zake yatapelekwa kwa msajili.
- Jumuiya tarajiwa itajaza fomu ya maelezo iliyotayarishwa na Msajili aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.
- Waombaji watalipia ada ya usajili kama itakavyopangwa na Halmashauri.
- Msajili atasajili Jumuiya iliyofuzu vigezo vinavyotakiwa.
- Baada ya usajili kukamilika, Msajili ataendelea na hatua ya kutangaza *COWSO* aliyosajili katika Gazeti la Serikali ili kutambuliwa rasmi.

4. MAKABIDHIANO YA CHETI

Baada ya taratibu za usajili kukamilika, Msajili atakabidhi cheti kwa Kamati Tendaji mbele ya Timu ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Wilaya na kisha Kamati Tendaji itaonyesha cheti hicho kwa wananchi wa eneo husika kwenye mkutano wa hadhara.

5. FAIDA ZA KUSAJILI *COWSO*

Miongoni mwa manufaa ambayo jamii itayapata kutokana na uundaji na usajili wa chombo huru cha Watumiaji Maji ni pamoja na:

i. Kuwa na Katiba inayoongoza uendeshaji wa mradi.
ii. Mradi kuwa mali ya wananchi walio wengi.
iii. Kuwa na uongozi thabiti na wenye sifa.
iv. Kuwajibika kwa viongozi katika kutoa taarifa ya mradi.

v. Miradi kuwa na fedha za uendeshaji na matengenezo.

vi. Kusimamia mapato yatokanayo na mauzo ya maji ili yatumike ipasavyo katika shughuli za uendeshaji na matengenezo, na pia kupanua miradi kwa lengo la kuboresha huduma kwa wananchi.

vii. Fedha zinazopatikana kutokana na mauzo ya Maji kutumika kwa ajili shughuli zinazohusu uendelevu wa huduma inayotolewa na miradi ya maji husika kwa manufaa ya Wananchi husika

6. MAJUKUMU YA *COWSO*

Yafuatayo ni majukumu ya Jumuiya za Watumiaji maji yakiwemo mengine kama yameainishwa kwenye Miongozo na Katiba ya Jumuiya za Watumiaji maji:-

- Msimamizi mkuu wa uendeshaji na matengenezo ya Miradi wao wa maji wanaoumiliki.
- Kukusanya mapato yanayotokana na huduma wanayotoa.
- Uandaaji wa taarifa za uendeshaji na usimamizi wa fedha katika Jumuiya yao.
- Kuhudhuria mikutano ya kijiji na Halmashauri.
- Kushiriki katika mipango yote inayohusu huduma ya maji.
- Kutoa ushauri kuhusu utungaji wa sera mbalimbali.
- Kuweka utaratibu unaofaa wa kutoa kiwango mahsusi cha huduma ya bure ya maji kwa watu wasiojiweza na makundi maalum kama itakavyokubalika katika jamii.
- Kutoa taarifa kuhusu shughuli zozote za kibinadamu zinazofanyika katika vyanzo ambazo zinaweza kuathiri utoaji wa huduma.
- Kutayarisha na kuratibu bajeti ya mapato na matumizi ya fedha za chombo cha watumiaji maji.
- Kuelimisha na kuwapa wananchi taarifa za mapato na matumizi, elimu ya afya na utunzaji salama wa maji.
- Kupendekeza bei ya maji.
- Kuishauri Serikali katika utungaji wa Sera inayohusiana na maendeleo na utunzaji wa vyanzo vya maji.
- Kutatua migogoro itakayojitokeza kwenye *COWSO*.

- Kuandaa na kutoa taarifa za mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka kwa wanachama wa *COWSO*, na nakala kutumwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa mujibu wa katiba.

7. UENDESHAJI WA *COWSO*

Kamati Tendaji itasimamia majukumu yote ya uendeshaji wa Jumuiya ya Watumiaji yaliyoainishwa hapo juu kulingana na Katiba ya Jumuiya ya Watumiaji Maji kuhakikisha huduma inakuwa endelevu kuzingatia kuwa:-.

- Matengenezo yanafanyika kwa wakati
- Gharama za uendeshaji zinatokana na mauzo ya maji.
- Kiwango cha bei ya maji kinakidhi gharama za uendeshaji na matengenezo.
- Fedha za Maji zinatumika kwa ajili ya shughuli za uendelevu wa Miradi ya Maji tu si vinginevyo.
- Kunakuwa na uhusiano mzuri kati ya Jumuiya ya Watumiaji maji na Serikali ya Kijiji.
- Kunakuwa uandaaji na uhifadhi wa taarifa za uendeshaji na matengenezo.
- Taarifa sahihi zinatolewa kwa Wananchi, Serikali ya Kijiji, Kata na Halmashauri
- Kunakuwa na mpango madhubuti wa uendeshaji na matengenezo.

8.0 HITIMISHO

(i) Ili miradi ya maji iwe endelevu na iweze kutoa huduma ya maji kwa ufanisi ni lazima iwe na fedha za kujiendesha zitakazotokana na mauzo ya maji. Hii itawezesha huduma ya maji kuwa endelevu. Sera ya maji inasisitiza miradi ijengwe, iendeshwe na kusimamiwa na wananchi ili ijiendeshe kwa kufanya matengenezo kila inapohitajika bila kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

(ii) Kila mradi wa maji ulioko kijijini ni lazima usajili kisheria Jumuiya ya watumiaji maji kitakachoendesha mradi huo. Lengo kuu la kuanzisha Jumuiya za watumiaji maji ni kuifanya miradi imilikiwe na kusimamiwa na wananchi wenyewe ili kuhakikisha huduma ya maji inakuwa endelevu.

(iii) Uanzishwaji na Uundwaji wa Jumuiya za Watumiaji Maji ufanywe na Wataalam wa ndani (*in-house facilitation*) endapo watatakiwa wataalam wa nje itabidi watumie mwongozo uliopo kwa usimamizi wa Halmashauri, Mkoa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

(iv) Kuwe na utaratibu/makubaliano ya kutoa motisha/posho kwa Watendaji wa Jumuiya za watumiaji maji ambao ni viongozi/wataalamu/watumishi (Mwenyekiti, Katibu, Mhazini, mafundi, wasimamizi wa vituo, n.k). Viwango vya posho/motisha

vioane na uwezo wa kifedha wa Jumuiya za watumiaji maji husika. Gharama za posho zote kwa mwezi zisizidi asilimia 20% za makusanyo yote ya mwezi husika.

9. VIAMBATISHO

Kiambatisho Namba 1: FOMU YA KUSAJILI

Water and Sanitation (Registration of Community Owned Water Supply Organisations) *GN. No. 21*

SCHEDULE

FORMS

FORM 1

(Regulation 9)

APPLICATION FOR REGISTRATION
COMMUNITY OWNED WATER SUPPLY ORGANISATION (COWSO)

(To be completed in triplicate)

To: The Registrar
……(Council)
P.O. Box……..
…….

Application is hereby made for registration of Community Owned Water Supply Organisation under the Water Supply and Sanitation Act.

1. Name of the community organization……
2. Category/ type of community organisation (state whether is a Water Consumer Association, Water Trust, NGO, Company etc)
   ……
3. The principal office of the community organization is situated at
   ……...
4. The postal address of the community organization……
5. In case the community organization has been registered under any other written law state the date of registration. The community organisation has been registered on the ……day of……..20 ……..
6. The purpose of the community organization are:

……..
……

7. We enclose herewith
   a. a copy of the constitution or memorandum of agreement of the association.
   b. minutes containing full names and signature of founder members.
   c. personal particulars of office bearers.
   d. an application fees.
   e. Other documents.
      ……..

Dated this ……day of ……..20……
Name and signature of two founding members
1.(Name) ……..2. (Name)…….
(Signature)…… (Signature)…….

Kiambatisho Namba 2: MFANO WA KATIBA

KATIBA

YA

JUMUIYA YA WATUMIAJI

MAJI WA ……
(taja eneo/sehemu)

……

(Taja mwezi na mwaka)

Angalizo: Mfano huu wa katiba, kanuni na taratibu unahusu uundaji wa Jumuiya za Watumiaji Maji; hauhusiki na aina zingine za vyombo kama vile Vyama vya Ushirika, Kampuni, Bodi ya Wadhamini, Mashirika yasiyo ya Kiserikali n.k. Katiba, kanuni, na taratibu za uundaji wa aina nyingine ya vyombo vya watumiaji maji utafuata sheria na kanuni zinazotawala vyombo hivyo.

DIBAJI

Kwa kutambua kuwa watumiaji maji wa (*taja eneo*) ---------- wanahitaji kuwa na Jumuiya cha kisheria cha kuendeleza na kusimamia huduma ya usambazaji wa maji kwa eneo la kijiji/vijiji vilivyo ndani ya mradi wa maji wa (*taja jina la mradi*) ---------- kwa madhumuni ya kuleta maendeleo na kustawisha ustawi wa jamii kwa ujumla.

Tumeamua kuanzisha Jumuiya ya Watumiaji Maji wa (*taja eneo*) ---------- ili kusimamia na kutunza mradi wa maji na vile vile kuendeleza juhudi na nia njema zilizokwishachukuliwa na vyombo pamoja na mamlaka mbalimbali katika eneo husika, kwa kuhamasisha vyanzo vya fedha mali ghafi na maendeleo ya jamii katika uelekeo huo.

Kwa hiyo Jumuiya itaongozwa kama inavyoeleza katika vipengele vifuatavyo:

SEHEMU YA KWANZA

1. Jina la Jumuiya na mahali ilipoandikishwa

1.1 Jina la Jumuiya litakuwa ----------

1.2 Anwani na makao makuu ni kijiji cha ---------- na Sanduku la barua ni S.L.P ----------.

1.3 Shughuli za Jumuiya ya Watumiaji Maji wa ---------- kwa ujumla zitaendeshwa na kusimamiwa na Kamati ya Uendeshaji.

SEHEMU YA PILI

2. Tafsiri na Ufafanuzi

2.1. Isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:

"**Katiba**" maana yake ni Katiba ya Jumuiya ya Watumiaji Maji wa ----------

"**Jumuiya**" maana yake ni Jumuiya ya Watumiaji Maji wa ----------

"**Eneo Tumia**" maana yake ni eneo lenye kuhudumiwa na tanki moja au eneo linalohudumiwa na tawi la bomba lililounganishwa kwenye bomba kuu la usambazaji maji.

"**Kundi Tumia**" maana yake ni kundi la watumiaji maji wanaochota maji kwenye kituo kimoja, taasisi au kituo binafsi.

"**Kanuni na Taratibu** "maana yake ni sheria ndogo ndogo zinazotawala uendeshaji wa jumuiya ya watumiaji maji.

"Mwanachama" maana yake ni taasisi au mtu yeyote ambaye amejiunga kwa hiari yake mwenyewe katika jumuiya ya watumiaji maji kwa mujibu wa katiba, na yuko tayari kutimiza masharti ya jumuiya.

SEHEMU YA TATU

3. Malengo na madhumuni ya Jumuiya yatakuwa:

3.1 Kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha kwa watumiaji.
3.2 Kukusanya fedha za utunzaji na matengenezo ya huduma ya maji.

3.3 Kusimamia na kufanya matengenezo ya kutosha kwenye mtego wa maji, bomba kuu, bomba la usambazaji na sehemu zote hadi kwenye vituo vya vinavyosimamiwa na Jumuiya *(vituo binafsi na taasisi havihusiki).*

3.4 Kushirikiana na jumuiya au vyombo vingine vya watumiaji maji katika eneo husika vyenye malengo na madhumuni yanayofanana na Jumuiya hii ya watumiaji maji wa ----------.

3.5 Kusimamia na kutunza maeneo ya ---------- ambayo ni chanzo cha maji kinachosimamiwa na jumuiya.

SEHEMU YA NNE
4. Uanachama wa Jumuiya

4.1 Aina za Uanachama

4.2

Kutakuwa na aina zifuatazo

(i) Wanachama wa kawaida
(ii) Wanachama washiriki au taasisi
(iii) Wanachama wa heshima

4.3 Kujiunga na mwisho wa Uanachama

Uanachama utapatikana kwa kila mmoja ili mradi tu ni mkazi kwenye eneo la mradi wa maji. Hakuna mwanachama yeyote anayeweza kusimamishwa au kufukuzwa uanachama.

Mwisho wa uanachama wa mwanachama ni hapo mtu anapohama eneo la mradi wa maji au anapokufa.

4.4 Mwisho wa upatikanaji wa huduma ya maji

Huduma ya maji itapatikana kwa mwanachama yule tu atakayekuwa ametimiza masharti kwa mujibu wa katiba kama vile kulipa ada, kiingilio, ada ya kadi na michango mingine.

4.5 Haki za mwanachama

(i) Kuhudhuria mikutano yote ya Jumuiya kama inavyoelekezwa na katiba, kushiriki na kujihusisha katika kupitisha maamuzi na maazimio katika mikutano
(ii) Kuhudhuria Mkutano Mkuu
(iii) Kupiga kura wakati wa uchaguzi wa viongozi wa Jumuiya
(iv) Kuchagua na kuchaguliwa kwenye nafasi yoyote ya uongozi wa Jumuiya.
(v) Taasisi, shirika na wanachama wa heshima, watumishi hawaruhusiwi kuchaguliwa katika nafasi yoyote ya uongozi wa Jumuiya hiki.

4.5 *Ada na michango*

4.5.1 Kila mtumiaji wa mradi wa maji wa ----------, anawajibika kulipa ada kama itakavyoamuriwa na Mkutano Mkuu.

4.5.2 Taasisi, mashirika na watu binafsi watalipa ada kama itakavyoamuliwa na mkutano Mkuu.

4.5.3 Wanachama wa heshima watatakiwa kulipa ada na kiingilio kama watavyoona.

4.5.4 Mtu yeyote anaweza kuchangia michango ya ziada.

SEHEMU YA TANO
5 Muundo wa Jumuiya

5.1 *Mpangilio wake*: Kutakuwa na mpangilio ufuatao wa Jumuiya

(i) Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Watumiaji Maji
(ii) Kamati ya Uendeshaji ya Jumuiya
(iii) Mkutano Mkuu wa Eneo Tumia
(iv) Kamati ya Uendeshaji ya Eneo Tumia

5.2. Mkutano Mkuu wa Jumuiya

5.2.1 Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya utakaofanyika mara moja kwa mwaka, mwezi ----------.

5.2.2 Kazi ya Mkutano Mkuu

(i) Kutoa maamuzi ya mwisho katika mambo yote yanayohusu Jumuiya kwa mujibu wa Katiba.
(ii) Kupitisha kanuni na taratibu za uendeshaji wa Jumuiya.
(iii) Kupitisha bajeti ya mapato na makadirio ya matumizi ya mwaka.
(iv) Kupokea na kupitisha taarifa ya fedha ya mwaka ya Jumuiya kutoka katika kamati ya uendeshaji.
(v) Kupokea taarifa mwaka ya maendeleo ya Jumuiya pamoja na matarajio ya siku za usoni.

5.2.3 Dondoo za Mkutano Mkuu zitakuwa kama zifuatazo:

(i) Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Muda
(ii) Kujadili na kupitisha taarifa ya mwaka
(iii) Kujadili na kupitisha bajeti

(iv) Uchaguzi wa kamati ya uendeshaji itakayokuwa madarakani kwa muda wa miaka mitatu. Baada ya hapo wagombea wanaomaliza muda wao wanaweza kugombea na kuchaguliwa tena.

5.2.4. Kiwango cha wajumbe wa Mkutano Mkuu kitakuwa ni asilimia 50 ya wajumbe wote wa Mkutano Mkuu.

5.2.5. Wajumbe watatu kutoka eneo tumia watahudhuria Mkutano Mkuu, ambao ni Mwenyekiti, Katibu na Mjumbe mmoja (wajumbe watabadilishana zamu za kushiriki).

5.2.6. Upigaji kura utafanyika kwa njia ya kura ya siri.

5.2.7. Kutakuwa na Mkutano Mkuu usiokuwa wa kawaida unaoweza kuitishwa iwapo asilimia 50 ya wajumbe wa kamati ya uendeshaji au wajumbe wa Mkutano wameomba kufanyika kwa Mkutano Mkuu. Idadi ya wajumbe ili mkutano ufanyike ni lazima iwe asilimia 50.

5.2.8. Taarifa ya mikutano yote itaitishwa na kamati baada ya kutoa taarifa ya maandishi ya siku saba (7).

5.3. Kamati ya Uendeshaji ya Jumuiya

5.3.1. Kamati ya Uendeshaji itakuwa na wajumbe wanane (8) watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya. Na kitakuwa ndicho chombo kikuu cha usimamizi na utekelezaji wa maamuzi yote ya Jumuiya.

5.3.2. Kazi za Kamati ya Uendeshaji.

(i) Kuandaa kanuni na taratibu na kuziwasilisha katika Mkutano Mkuu ili zijadiliwe na kupitishwa.

(ii) Kupokea taarifa ya nusu mwaka ya Mtunza Fedha na kuiwasilisha katika Mkutano Mkuu wa Jumuiya. Taarifa ya mwaka ya Mtunza Fedha ni lazima iwe imekaguliwa na wakaguzi wanaotambuliwa kisheria.

(iii) Kupendekeza kwenye Mkutano Mkuu viwango vya malipo ya maji, ada ya Uanachama na michango mingine.

(iv) Kuajiri, kumsimamisha kazi au kumwondoa Meneja wa Jumuiya.

(v) Kuajiri, kumsimamisha kazi au kumwondoa Mtunza Fedha wa Jumuiya.

(vi) Kuajiri, kuwasimamisha kazi au kuwaondoa mafundi, mawakala na walinzi wa Jumuiya.

NB: Ikibidi kamati inaweza kuvunjwa, na wajumbe wasiowajibika wanaweza kubadilishwa kabla ya muda wa miaka mitatu kumalizika.

5.3.3. Mikutano ya Kamati ya Uendeshaji.

i) Mkutano wa kamati ya uendeshaji utafanyika kila robo mwaka, mwezi wa tatu, sita, tisa na kumi na mbili.

ii) Mkutano Mkuu wa kamati ya uendeshaji utakuwa chini ya Mwenyekiti wa Kamati.

iii) Kiwango cha wajumbe kwenye kikao cha kawaida cha kamati ya uendeshaji kisipungue wajumbe watano (5), Mwenyekiti au Katibu wasipokuwepo atateuliwa mjumbe mmoja kushika nafasi hiyo kwa muda na maamuzi yatafikiwa kwa wingi wa kura.

5.3.4 Dondoo za Vikao vya Kamati ya Uendeshaji
(i) Uchaguzi wa Mwenyekiti na Katibu *(pale inapotakiwa)*
(ii) Uchaguzi wa wajumbe watatu wa kamati mbali mbali *(pale inapotakiwa)*
- Kamati ya Mipango, Fedha na Elimu.
- Kamati ya Ufundi na Ulinzi.

(iii) Kupokea taarifa ya Meneja kuhusu uendeshaji wa mradi
(iv) Kupokea taarifa ya Mtunza Fedha.
(v) Kukubaliana kuhusu makisio ya bajeti na kuwakilisha kwenye Mkutano Mkuu ili iidhinishwe.
(vi) Mengineyo.

5.4. Ngazi ya Eneo Tumia

Muundo wa usimamizi katika eneo tumia utakuwa kama ifuatavyo:
(i) Mkutano mkuu wa watumiaji wanachama katika ngazi ya eneo tumia.
(ii) Kamati ya uendeshaji ya eneo tumia itakuwa na wajumbe sita (6).

5.5. Mkutano Mkuu wa Eneo Tumia

Ratiba na taratibu za mkutano mkuu wa eneo tumia utakuwa kama ifuatavyo:
(i) Mkutano Mkuu wa eneo tumia utafanyika mara 2 kwa mwaka mwezi ---------- na ----------.
(ii) Kiwango cha wajumbe wa Mkutano mkuu kitakuwa sio chini ya asilimia 50 ya wajumbe wote wa Mkutano Mkuu.
(iii) Mkutano mkuu wa eneo tumia utaitishwa kwa kutoa taarifa ya siku 7 kwa maandishi.
(iv) Upigaji kura utafanywa kwa njia ya kura ya siri.
(v) Kutakuwa na Mkutano Mkuu usiokuwa wa kawaida unaoweza kuitishwa iwapo asilimia 50 ya wajumbe wa kamati ya uendeshaji au wajumbe wa mkutano wameomba kufanyika kwa Mkutano Mkuu (idadi ya wajumbe ili mkutano ufanyike ni lazima iwe asilimia 50 au zaidi).

5.5.1. Kazi za Mkutano Mkuu wa Eneo Tumia
Mkutano mkuu wa eneo tumia utakuwa na kazi zifuatavyo:
(i) Kuchagua wajumbe wa kamati ya uendeshaji ya eneo tumia.
(ii) Kupokea taarifa ya fedha ya mwaka ya eneo tumia.
(iii) Kupokea taarifa ya maendeleo ya mradi ya mwaka.

5.5.2. Dondoo za Mkutano Mkuu wa Eneo Tumia.
(i) Kuchagua mwenyekiti wa mkutano.
(ii) Kuchagua wajumbe wa kamati ya uendeshaji ya eneo tumia ambao muda wao umemalizika.
(iii) Kupokea na kuijadili taarifa ya utekelezaji ya mwaka
(iv) Kupokea na kuijadili taarifa ya fedha
(v) Mengineyo.

5.6. Kamati ya Uendeshaji ya Eneo Tumia.

Kamati ya uendeshaji ya eneo tumia itakuwa na wajumbe 6 ambao watachaguliwa na mkutano mkuu wa eneo tumia kila baada ya miaka mitatu. Wajumbe watawajibika kwa mkutano mkuu wa eneo tumia.

5.6.1. Kazi za Kamati ya Uendeshaji ya Eneo Tumia

Kamati ya uendeshaji ya eneo tumia itakuwa na kazi zifuatazo.

(i) Kutoa mapendekezo ya kwenye bajeti ya Jumuiya
(ii) Kuwahamasisha watumiaji maji kulipia malipo ya maji, viingilio, ada za uanachama na michango mingine.
(iii) Kuwahamasisha watumiaji maji kujiunga na Jumuiya
(iv) Kuitisha mkutano mkuu wa eneo tumia.

5.6.2. Vikao vya Kamati ya Uendeshaji ya Eneo Tumia

Ratiba na taratibu za kamati ya uendeshaji ya eneo tumia vitakuwa kama ifuatavyo:

(i) Vikao vya kamati ya uendeshaji ya eneo tumia vitafanyika mara nne kwa mwaka katika mwezi wa tatu, sita, tisa na kumi na mbili.
(ii) Wajumbe wa kamati ya eneo tumia watakuwa si chini ya wanne. Kama Mwenyekiti na katibu hawakuhudhuria, wajumbe wawili watachaguliwa ili kushika nafasi hizo kwa muda. Maamuzi yatafikiwa kwa wingi wa kura.
(iii) Uchaguzi wa dharura utaitishwa ikibainishwa kwamba, wajumbe wa kamati ya uendeshaji ya eneo tumia hawatawajibika na kuchagua wajumbe wengine.

5.6.3 Dondoo za Vikao vya Eneo Tumia

(i) Kuchagua mwenyekiti na katibu (pale itakapohitajika)
(ii) Kupokea taarifa kutoka kwa wajumbe kuhusu kazi walizopewa
(iii) Kupokea taarifa ya utekelezaji ya wakala/mkusanyaji
(iv) Mengineyo.

SEHEMU YA SITA

6. Viongozi Wakuu wa Jumuiya ya Watumiaji Maji

6.1 Kutakuwa na Viongozi wakuu wawili wa Jumuiya ambao ni Mwenyikiti na Katibu.
6.2 Mali zote za Jumuiya zitasimamiwa na wanachama wa Jumuiya na zitakuwa mikononi mwao.
6.3 Viongozi watakuwa na mamlaka ya kisheria ya kushitaki na kushitakiwa kwa niaba ya Jumuiya kwa mujibu wa sheria na katiba.
6.4 Viongozi wakuu watakuwa na uwezo ufuatao wa kiutendaji katika Jumuiya:

(i) Kupokea misaada kutoka sehemu nyingine yoyote
(ii) Kukopa kutoka benki au taasisi au kikundi kingine au sehemu yoyote kwa niaba ya Jumuiya na baada ya makubaliano kwa ajili ya kuendesha mradi.
(iii) Kupanga au kupangisha.
(iv) Kukopa au kukopesha katika vyombo vingine.
(v) Kuweka rehani samani za Jumuiya.

NB: Viongozi hao watafanya yote hayo hapo juu baada ya kushauriana na kamati ya uendeshaji baada ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya.

SEHEMU YA SABA

7. Vyanzo vya Mapato vya Jumuiya

7.1 Jumuiya ya watumiaji maji wa ---------- itakuwa na vyanzo vya mapato kama ifuatavyo.

(i) Malipo ya maji kutoka kwa watumiaji wa ndani na nje ya Jumuiya.
(ii) Malipo ya maji kutoka kwa wafugaji
(iii) Malipo ya maji kutoka kwenye taasisi na vituo binafsi
(iv) Malipo kutokana na adhabu mbalimbali
(v) Viingilio vya uanachama pamoja na ada za wanachama
(vi) Mauzo ya kadi
(vii) Ruzuku au zawadi kutoka Jumuiya au taasisi nyingine
(viii) Njia nyingine yoyote halali
(ix) Mauzo ya mali za Jumuiya.

SEHEMU YA NANE

8. Marekebisho ya Katiba

8.1 Hakuna kitu chochote katika katiba hii kitakachorekebishwa, isipokuwa katika Mkutano Mkuu ambao utakuwa umeitishwa maalum kwa ajili hiyo, ambapo asilimia 50 ya wajumbe wote watakubaliana kufanya marekebisho hayo.

SEHEMU YA TISA

9. Kanuni na Taratibu

9.1 Jumuiya ya Watumiaji Maji itatunga kanuni na taratibu za uendeshaji wa Jumuiya zitakazopitishwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya kama ilivyoainishwa katika kifungu Na. 5.2.2.(ii)

SEHEMU YA KUMI

10. Walezi wa Jumuiya

10.1 Viongozi wafuatao wa Wilaya watakuwa ndio Walezi wa Jumuiya:

(i) Mkuu wa Wilaya
(ii) Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya

10.2. Walezi watakuwa washauri wa Jumuiya

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

11. Wadhamini wa Jumuiya cha Watumiaji Maji

11.1. Wafuatao watakuwa ni wadhamini wa Jumuiya:

(i) ---------- (vi) ----------

(ii) ---------- (vii) ----------

(iii) ---------- (viii) ----------

(iv) ---------- (ix) ----------

(v) ---------- (x) ----------

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

12. Mengineyo

12.1. Bila kuathiri yaliyomo katika katiba hii iwapo kutatokea ubishi wa tafsiri na ufafanuzi katika vipengele vya katiba, basi tafsiri ya kiingereza itatumika.

12.2. Katiba hii itatumika mara baada ya kukubaliwa na kupitishwa na angalau asilimia 50 ya wanachama wote wenye haki ya kupiga kura katika Mkutano Mkuu wa kwanza mara baada ya Jumuiya kusajiliwa.

Katiba hii ni kama ilivyopokelewa na kukubaliwa na wanachama waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Watumiaji Maji wa ----------uliofanyika tarehe----------

Katiba hii imesainiwa na Kamati ya Uendeshaji ilivyochaguliwa kwa mara ya kwanza kwa niaba ya Jumuiya ya Watumiaji Maji wa ---------- kama ifuatavyo:

---------- ----------

1. Mwenyekiti Tarehe

---------- ---------- ----------

2. Katibu Tarehe

---------- ----------

3. Mjumbe Tarehe

Kiambatiusho Namba 3: KANUNI NA TARATIBU ZA JUMUIYA YA WATUMIAJI MAJI

KANUNI NA TARATIBU

ZA

CHOMBO CHA WATUMIAJI WA MAJI

WA ENEO LA----------

Kinachotambulika kwa Jina la

(Jina la Chombo cha Watumiaji Maji)

(Mwezi, Mwaka)

Kiambatisho Namba 3 KANUNI NA TARATIBU

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA NA. 12 YA 2009 NA KANUNI ZA USAJILI WA VYOMBO VYA WATUMIAJI MAJI ZILIZOTANGAZWA KATIKA GAZETI LA SERIKALI NA. 21 TAREHE 22/1/2010

1. KANUNI YA KWANZA

1.1. Kanuni na taratibu hizi zitajulikana kama sheria ndogo ndogo za chombo cha watumiaji maji wa (*taja eneo*) ---------- ambacho kinatambulika kwa jina la ----------.

2. KANUNI YA PILI

2.1. Madhumuni ya Chombo
2.2. Kinaanzishwa chombo cha watumiaji maji ambacho kitajulikana kwa jina la ---------- ---------- *(jaza jina la eneo husika)*
2.3. Chombo hiki na kamati zake kitakuwa na uwezo, mamlaka na madaraka ya kisheria na katika wadhifa huo kitakuwa na uwezo wa kushitaki au kushitakiwa.
2.4. Kuendeleza haki ya kutumia maji na kuhakikisha kuwa maji yanapatikana muda wote kwa watumiaji maji wa eneo la ----------
2.5. Kulinda, kuhifadhi na kutunza maeneo ya ---------- ambayo ni chanzo cha maji ya kinachosimamiwa na chombo.
2.6. Kushirikiana na mamlaka nyingine zinazohusika kuweka mikakati ya kufanya marekebisho, kupanua huduma za maji au kazi nyingine ambazo zitajitokeza wakati wowote ule endapo itakuwa ni muhimu kwa madhumuni yatakayofaa kwa uendelezaji wa huduma ya maji.

3 KANUNI YA TATU

3.1 Ili kuweza kutekeleza madhumuni na shabaha za chombo kama ilivyoelekezwa na katiba ya chombo sehemu ya tatu kuanzia kifungu cha 3.0 (3.1-3.5) chombo kitatekeleza yafuatayo:

3.1.1 Chombo kitaweka mipango na kufuata taratibu za uendeshaji na kutunza mazingira ya vituo vyote vya usambazaji maji ----------
3.1.2 Chombo kitafanya shughuli zote ambazo ni halali kisheria na kuchukua hatua za kisheria pale ambapo itaona inafaa kwa madhumuni ya chombo au kwa manufaa ya Jamii.
3.1.3 Kuajiri kwa masharti na mapatano ambayo kamati ya uendeshaji itaona inafaa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za chombo. Pia kutoa mwongozo wa madhumuni yake, au kumsimamisha, au kumwachisha yeyote endapo atakuwa yuko kinyume na wajibu wake, kama ilivyo kwenye sehemu ya tano kifungu cha 5.3.2 (iv-vi) ya katiba ya chombo.
3.1.4 Kuweka raslimali ya fedha na mali nyingine za chombo ambazo hazitahitajika mara moja katika shughuli nyingine kama itakavyopendekezwa na kamati ya uendeshaji.

3.2 Wenye Ofisi na Kamati ya Uendeshaji kushughulikia madeni, kukopa fedha kwa kiasi kulingana na shughuli na kwa masharti kama itakavyoshauriwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu kifungu cha 6.4 (ii) na (iv) cha katiba.

3.3 Chombo kitatunza kitabu cha orodha ya uanachama ambacho kitakuwa chini ya uangalizi wa kamati ya uendeshaji.

4 KANUNI YA NNE

4.1 Uanachama, Haki na Wajibu
Wanachama wote watatakiwa kutimiza wajibu unaowapasa, na pia watakuwa na haki zao kwa mujibu wa katiba.

4.2 Chombo kitakuwa na wanachama wa aina tatu
(a) Mwanachama wa Kawaida
(b) Taasisi au Shirika
(c) Mwanachama wa heshima kama ilivyo katika sehemu ya kifungu cha 4.1 cha Katiba.

4.2 (a) *Mwanachama wa Kawaida*

(i) Mwanahama wa kawaida ni mtu yeyote ambaye umri wake ni miaka 18 na kuendelea, mwenye akili timamu.

(ii) Mtu yeyote mwenye akili timamu aliyetimiza sharti la katiba ya kifungu cha 4.2.1 na anatumia maji yanayosimamiwa na chombo, moja kwa moja atakuwa mwanachama wa chombo.

(iii) Baada ya kuwa mwanachama wa kawaida, itamlazimu kulipa ada ya kiingilio ambayo itaamuliwa katika kikao cha kwanza cha Mkutano Mkuu wa mwaka.

4.2 (b) *Mwanachama Mshiriki au Taasisi*

(i) Uanachama wa Taasisi au Shirika la umma, Kampuni binafsi, Chombo kingine au Taasisi za Madhehebu ya dini ambayo yanafanya kazi katika eneo la ----------, uanachama unapatikana kwa maombi.

(ii) Mwombaji wa uanachama wa Shirika/Taasisi atatakiwa kutoa maelezo katika mambo yanayohusiana na huduma anayoitoa.

(iii) Atakapo kubaliwa kuwa mwanachama atalipa ada au kiingilio kwa kiasi ambacho kitakuwa kimepangwa/kukadiriwa katika Mkutano Mkuu wa kamati ya uendeshaji na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu.

(iv) Wanachama wa Shirika/Taasisi hawatachaguliwa kushika nafasi yoyote ya uongozi wa chombo.

4.2 (c) *Uanachama wa Heshima*

(i) Mwanachama wa heshima atakuwa mtu yeyote atakayependekezwa na kamati ya uendeshaji na kuchaguliwa katika Mkutano wowote wa mwaka kwa kuzingatia jinsi alivyochangia au nafasi aliyonayo kwa faida na manufaa ya chombo.

(ii) Mwanachama wa Heshima ni lazima awe mtu mwenye maadili mazuri na kukubalika na jamii.

(iii) Mwanachama wa heshima akishapewa uanachama atalipa kiingilio na ada kiasi chochote atakachoweza.

(iv) Mwanachama wa heshima hatachaguliwa kushika nafasi yoyote ya uongozi wa Chombo.

5.0 KANUNI YA TANO

5.1. Muundo na Madaraka ya Chombo

5.2 *Chombo hiki kimeundwa katika ngazi tatu:*

(a) Kundi Tumia

(b) Eneo Tumia

(c) Chombo cha Watumiaji Maji

5.2 (a) **Ngazi ya Kundi Tumia**

(i) Hii itajumuisha watumiaji wa kituo kimoja cha kuchotea maji (DP) na taasisi au kituo binafsi.

5.2 (b) **Ngazi ya Eneo Tumia**

(i) Hii itajumuisha makundi tumia yaliyounganisha kutoka tenki moja, au eneo linalohudumiwa toka bomba kuu.

(ii) Katika ngazi ya eneo tumia kutakuwa na Mkutano Mkuu ambao utahudhuriwa na watumiaji maji wote. Katika eneo tumia na kila mwanachama atakuwa na haki ya kupiga

kura wakati wa uchaguzi na watachaguliwa wajumbe 6 wa kamati ya uendeshaji ya eneo tumia (jinsia izingatiwe)

5.2 (c) **Ngazi ya Chombo**

(i) Hii itajumuisha maeneo tumia yote na makundi tumia yote.
(ii) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chombo ni kama ilivyo kwenye sehemu ya tano kifungu cha 5.3.
(iii) Kwenye Mkutano Mkuu watachaguliwa wajumbe 8 wa kamati ya uendeshaji ya Chombo.
(iv) Majukumu ya kamati ya uendeshaji yameonyeshwa kwenye sehemu ya tano kifungu cha 5.5.5 cha Katiba ya Chombo.
(v) Mkutano Mkuu wa kawaida wa Chombo utaongeza idadi ya wajumbe wa kamati ya uendeshaji kulingana na hali ya kiofisi au kupanuka kwa shughuli za Chombo.
(vi) Kabla ya Mkutano Mkuu kuanza, mkutano utamchagua Mwenyekiti wa muda miongoni mwa wajumbe. Na madaraka Mwenyekityi huyo yatamalizika mara baada ya mkutano huo kumalizika.

6. KANUNI YA SITA

Inatokana na sehemu ya saba ya katiba.

6.1 Vyanzo vya Mapato na Mali za Chombo

6.2 Chombo cha Watumiaji maji wa ---------- itakuwa na vyanzo vya mapato na mali kama ifuatavyo:
(i) Mapato kutokana na mauzo ya maji na adhabu mbalimbali.
(ii) Ada ya viingilio vya wanachama.
(iii) Michango ya hiari kama itakavyoamuliwa na Mkutano Mkuu.
(iv) Ruzuku/zawadi kutoka Vyombo vingine vinazofanana na Chombo hiki, watu binafsi, vyama vya hiari, taasisi, Idara za serikali nje na ndani ya nchi.
(v) Njia nyingine halali itakavyopendekezwa na kamati ya uendeshaji na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu.
(vi) Mali ya Chombo

7. KANUNI YA SABA

7.1. Matumizi ya Maji yanayosimamiwa na Chombo
Maji yanaweza kutumika kwa shughuli za nyumbani, za kunyweshea mifugo, kuogesha mifugo, bustani ndogondogo na shughuli nyingineza maendeleo ya mwanachama kinachotakiwa ni yule mtumiaji alipie kulingana na kiasi cha maji kilichotumika.

8. KANUNI YA NANE

Miongoni mwa kazi za Kamati ya Utekelezaji ni pamoja na masuala ya ajira za wafanyakazi na hitimisho la ajira hizo kama inavyoelezwa katika kifungu cha 5.3.2. (iv-vi) cha katiba.

8.1 Waajiriwa kwenye Chombo
Ili kufanikisha shughuli za usimamizi na uendeshaji, wa chombo, chombo kitaajiri watumishi wafuatao kulingana na mahitaji yake

(a) Meneja

(b) Mtunza Fedha

(c) Wakala

(d) Mafundi

(e) Walinzi

8.1.1 (a) **Meneja**

(i) Ataajiriwa na Kamati ya Uendeshaji kwa kujaza mkataba maalum.
(ii) Meneja anaweza kusimamishwa kazi endapo atakuwa ameshindwa kutekeleza wajibu wake kama inavyoonyeshwa sehemu ya tano kifungu 5.3.2. (iv) cha Katiba ya Chombo.
(iii) Meneja atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu na Msimamizi wa waajiriwa wengine wote wa Chombo.
(iv) Atatoa mapendekezo na makisio ya mapato na matumizi ambayo yatajadiliwa na kamati ya uendeshaji.
(v) Atatekeleza kazi nyingine zote za Chombo atakazopangiwa na kamati ya uendeshaji.

8.1.2 (b) **Mtunza Fedha**

(i) Ataajiriwa na kamati ya uendeshaji na kujaza mkataba maalum.
(ii) Atapokea malipo ya maji na michango mbalimbali ya wanachama toka kwa mawakala wa maeneo tumia, fedha taslimu, hundi na nyaraka mbalimbali.
(iii) Atatumia hati za malipo na stakabadhi ya fedha kwa fedha yote inayopokelewa na kutolewa.
(iv) Fedha zote za Chombo zitatunzwa benki, ambayo kamati ya uendeshaji itachagua kutunzia fedha. Fedha zitachukuliwa kwa hundi iliyotiwa saini na aidha Mwenyekiti au Katibu, kama mtia sahihi daraja la kwanza na Meneja au Mtunza fedha mtia sahihi daraja la pili.
(v) Atahudhuria vikao vya kamati na mikutano yote ili kusaidia kufafanua na kutafsiri nyaraka na kumbukumbu ya hesabu za Jumuiya.
(vi) Ataandaa taarifa ya mapato na matumizi kwa vipindi vya miezi mitatu mitatu kwa kusaidiana na meneja.
(vii) Mtunza fedha anaruhusiwa kuwa na fedha mkononi kwa matumizi ya dharura kiasi cha Tsh. ----------kulingana na maamuzi ya kamati ya uendeshaji.

8.1.3 (c) **Wakala wa Chombo**

(i) Ataajiriwa na Kamati ya Uendeshaji ya Chombo
(ii) Atakusanya mapato yote yatokananyo na mauzo ya maji kwenye eneo tumia na kuziwasilisha fedha kwa Mtunza Fedha wa Chombo.
(iii) Atatoa taarifa kwa wanachama wa eneo tumia kuhusu maendeleo ya kifedha ya Chombo.
(iv) Atafanya kazi nyingine zote atakazopangiwa na Mtunza Fedha wa Chombo
(v) Atatekeleza mambo yote yaliyomo kwenye mkataba wa ajira yake.

8.1 4 (d) **Mafundi/Wahudumu**

(i) Wataajiriwa na kamati ya uendeshaji ya Chombo

(ii) Kila fundi atafanya matengenezo ya kawaida na ya kinga katika eneo tumia atakalopangiwa na meneja.

(iii) Atasimamia shughuli zote za matengenezo na kutunza vifaa vyote vya ufundi bomba.

(iv) Atashauriana na Meneja juu ya masuala ya ki-ufundi pale itakapolazimu kufanya hivyo.

8.1.5 (e) **Walinzi**

(i) Wataajiriwa na kamati ya uendeshaji ya Chombo

(ii) Watalinda eneo lote la vyanzo vya maji (Intake)

(iii) Watatoa taarifa ya uharibifu uliojitokeza wakati wote kwa Meneja wa Chombo.

(iv) Watatekeleza mambo yote yaliyomo kenye mkataba wa ajira yao.

9. KANUNI YA TISA

9.1 Marekebisho ya Katiba ya Chombo

(i) Marekebisho ya Katiba yatafanywa kutokana na maazimio ya Mkutano Mkuu ambao utakuwa kwa ajili hiyo.

(ii) Marekebisho ya Katiba yatafanywa endapo kwenye Mkutano Mkuu maazimio yatakuwa yamepigiwa kura na asilimia 25% ya wajumbe wote wenye haki ya kupiga kura.

10. KANUNI YA KUMI

10.1 Kutakuwa na walezi na wadhamini wa chombo kama ilivyoonyeshwa kwenye sehemu ya kumi na sehemu ya kumi na moja ya Katiba ya Chombo.

10.2 Maeneo tumia yafuatayo ndiyo yanayounda chombo cha watumiaji maji wa ----------.

No.	Eneo Tumia	Tarafa	Kata
1			
2			
3			
4			
5			
6			

Kanuni na taratibu hizi zimepokelewa na kukubaliwa na wanachama waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Chombo cha ----------uliofanyika tarehe ----------.

---------- ----------

Sahihi ya Mwenyekiti Tarehe

---------- ----------

Sahihi ya Katibu Tarehe

---------- ----------

Sahihi ya Mjumbe Tarehe

Kiambatisho Namba 4. MFANO WA CHETI

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji

CHETI CHA USAJILI

Namba ya Cheti: ……

Hii ni kuthibitisha kwamba, Leo tarehe……..mwezi…….mwaka

Mimi …….kwa mamlaka niliyopewa chini ya Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2010, nathibitisha kwamba ..... imesajiliwa rasmi chini ya kifungu Na 34 (1) cha sheria hii. Chombo hiki kitajulikana kama:

Jina: …….

Anwani : ……..

.....

Namba ya Simu ……..

Eneo la Huduma litakalosimamiwa……..

Taja majina mengine ya kijiji/vijiji ……..…au Kata / Tarafa zitakazohusika kama zipo)

Imetolewa leo tarehe …… (Eleza majina ya mwezi na